
# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# PROGRAMU TUMIZI YA ANWANI ZA MKAZI




WASILISHO KWA MTUMIAJI
( MKUSANYA TAARIFA)

# YALIYOMO

1. Utangulizi ........................................................................ 1

2. Dashibodi ........................................................................ 2

2.1 Kusajili Anwani ........................................................................ 3

2.1.1 Usajili wa Anwani Kuu ........................................................................ 3

2.1.2 Anwani zilizosajiliwa ........................................................................ 4

# 1. UTANGULIZI

Mfumo wa  Anwani za Makazi ni Muundombinu unaotambulisha mtu alipo, anapopatikana ama anapotakiwa kuhudumiwa; nyumbani, ofisini ama eneo la biashara.
Mfumo wa Anwani za Makazi una manufaa mengi kiuchumi na kijamii. Manufaa hayo ni pamoja na:-


1. Hutoa Anwani ya Makazi kwa kila mwananchi ama mkazi katika eneo lake la nyumbani, ofisini ama biashara hivyo kumtambulisha mwananchi mahali alipo ama anapohitaji kuhudumiwa;
2. Hurahisisha shughuli za kutafuta na kupokea huduma na bidhaa;
3. Hurahisisha shughuli za kutoa na kupeleka huduma ama bidhaa mahali stahiki;
4. Huongoza kwa urahisi ama bila usumbufu kutoka eneo moja (Anwani moja ya Makazi) kwenda eneo jingine (Anwani nyingine ya Makazi);
5. Huwezesha kufanyika kwa biashara mtandao;
6. Hutoa taarifa ya msingi ya utambuzi;
7. Huwezesha kupanga na kutekeleza mipango kwa tija na ufanisi;
8. Huongeza tija katika huduma za uokoaji na maafa;
9. Huimarisha ukusanyaji wa mapato;
10. Huongeza ajira hususan za kupeleka barua, nyaraka na bidhaa nyumbani, ofis ini ama eneo la biashara;
11. Huimarisha ulinzi na usalama; na
12. Hufanikisha kazi za tafiti mbalimbali.
13. 
14. 

**LENGO LA WASILISHO**

Mfumo wa Anwani za makazi unatekelezwa kwa ajili ya kutoa Anwani ya Makazi ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji na utoaji wa huduma kwa wananchi. Mfumo huu una uweza kutumiwa na taasisi mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuunganishwa na mifumo mingine kwa ajili ya kubadilishana taarifa zinazohitajika. Kutokana na uwezo wa mfumo kubadilishana taarifa tunapenda kuunganisha mifumo kutoka taasisi mbalimbali za serikali ambayo tayari ina taarifa zinazohitajika katika zoezi la awali la  usajili wa anwani za makazi. Mifumo hiyo ni kama vile NIDA, TRA, ILMIS, BRELA.


Kwa kuwa serikali inatengeneza National Enterprise Service Bus (NESB) ambayo inaunganisha mifumo tajwa hapo juu, NaPA ingependa kubadilishana taarifa hizo kwa madhumuni ya usajili sahihi wa taarifa za anwani za makazi.

1. Bonyeza icon ya NaPA kwenye menyu ya simu yako.
2. ingiza barua pepe yako uliyosajiliwa nayo, jaza nywila yako kisha bonyeza kitufe cha ingia kuingia ndani ya programu.
Uingiapo kwenye mfumo moja kwa moja itakupeleka kwenye dashibodi kama ionekanavyo kwenye picha namba 3.




## 2. Dashibodi

1. ***“Usimamizi wa anwani”*** - Usajili wa anwani kwenye mfumo.
2. ***“Anwani zilizosajiliwa”*** kuona anwani zilizosajiliwa kwa hatuwa zote **“Anwani nje ya Seva” “Anwani kwenye Seva”.**
3. ***“Anwani kwenye Seva” -*** Anwani zilizo toka kwenye simu ya mkusanya taarifa na kutumwa kwenye seva ya mfumo wa napa.
4. ***“Anwani nje ya Seva”*** - Anwani zilizopo kwenye simu yamkusanya taarifa ila hazipo kwenye seva ya mfumo wa napa.
5. ***“Anwani kwa mhakiki”*** - Anwani zilizo kamilika na kutumwa kwa mhakiki.
6. “***Anwani zilizokubalika” -*** anwani zilizopitishwa na mhakiki.
7. “***Onesha upya dashbodi” -*** kurefreash dashboad
8. Bonyeza kuona taarifa za mkusanyaji



Muendelezo wa maelezo ya Dashibodi

9. **Bonyeza menyu yenye vidoti vitatu kuona**

**i. Mpangilio**

kurahisisha utafutaji, wa usalama (kubadili nywila), Maelezo na matumizi ya mfumo ikiwemo ubadilishaji wa lugha

**ii. Vuta barabara**


zilizoongezwa kwenye mfumo bila kutoka katika programu

**iii. Pakua aplikesheni mpya**

programu iliyo sasishwa

**iv. Toka**


kutoka nje ya programu




## 2.1 KUSAJILI ANWANI

### 2.1.1 Usajili wa Anwani kuu

Bonyeza ***"Usimamizi wa anwani"*** katika dashibodi yako kutajaza taarifa za anwani kuu. bonyeza alama ya kamera kuchukua usahihi wa alama za nukta usiozidi mita 4.





**NB:**
Uwanja wenye (*) ni lazima kujaza, kisha bonyeza **endelea** kujaza taarifa za huduma, jengo tegemezi, mmiliki na wategemezi wa anwani.











## 2.1.2 Anwani zilizosajiliwa

Bonyeza kitufe cha anwani zilizosajiliwa kuona orodha anwani zilizosajiliwa kwenye mfumo.



Bonyeza ***Kwenye mchakato*** kuona anwani

**1. zilizohifadhiwa**,


anwani ambazo zimehifadhiwa kwenye seva ya mfumo wa NaPA


**2. zinazohakikiwa**


anwani ambazo zimethibitishwa kukamilika zikatumwa kutoka kwenye seva kwenda kwa mhakiki

**3. zilizokubalika**


anwani baada ya kuhakikiwa na mhakiki na kukubalika




kwenye anwani zilizo hifadhiwa bonyeza kitufe cha wasilisha data , kupeleka taarifa kwenye kanzidata kwaajili ya uhakiki.





**Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**
**Anwani za Makazi**
**Barua pepe: napa@mawasiliano.go.tz**
**Tovuti: napa.mawasiliano.go.tz**
**Instagram: napa_tanzania**
**Twitter: napa_tanzania**
**Youtube: NAPA TV**